# WIZARA YA KILIMO

# KAULI YA SERIKALI KUHUSU KUIBUKA KWA UGONJWA MPYA KWENYE ZAO LA KOROSHO ILIYOTOLEWA BUNGENI NA MHE. MHANDISI DKT. CHARLES JOHN TIZEBA (MB), WAZIRI WA KILIMO

**18 APRILI, 2018**

## KAULI YA SERIKALI KUHUSU KUIBUKA KWA UGONJWA MPYA KWENYE ZAO LA KOROSHO ILIYOTOLEWA BUNGENI NA MHE. MHANDISI DKT. CHARLES JOHN TIZEBA (MB), WAZIRI WA KILIMO TAREHE 18 APRILI, 2018

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kanuni Namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu tatizo la kuwepo kwa ugonjwa wa MNYAUKO FUSARI kwenye zao la korosho katika mikoa ya Pwani, Mtwara na Lindi.

### HALI YA UZALISHAJI WA ZAO KOROSHO NCHINI

**Mheshimiwa Spika**, Zao la Korosho ni miongoni mwa mazao muhimu ya biashara yanayowanufaisha wakulima na kuchangia katika uchumi wa Taifa. Katika msimu wa mwaka 2017/2018 zao hili limeliingizia Taifa mapato ya kiasi cha shilingi trilioni 1,189,412,498,433.

**Mheshimiwa Spika**, Zao la korosho linalimwa kwa wingi katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga. Mikoa mingine inayolima zao hili ni Morogoro, Iringa, Mbeya, Singida na Dodoma. Inakadiriwa kwamba zaidi ya kaya 500,000 zinajihusisha na kilimo cha korosho na kila kaya ina wastani wa hekta 2 za shamba la korosho. Aidha, inakadiriwa kwamba Tanzania kuna mikorosho ipatayo milioni 50 yenye uwezo wa kutoa wastani wa kilo 5 kwa mti. Uwezo huu wa uzalishaji ni mdogo ikilinganishwa na miti ya mikorosho yenye matunzo bora inayotoa wastani wa kilo 15 mpaka 20.

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa uzalishaji wa korosho unaonesha kuna kupanda na kushuka kwa uzalishaji kutoka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, msimu wa 2014/2015 uzalishaji ulikuwa tani 197,932.501, msimu 2015/2016 tani 154,335, msimu 2016/2017 tani 265,237 na 2017/2018 tani 313,053.7

## KUIBUKA KWA UGONJWA MPYA KWENYE ZAO LA KOROSHO

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Wizara ya Kilimo imepokea taarifa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele kuhusu kuwepo kwa ugonjwa huo kwenye mikoa tajwa hapo juu. Taasisi ya Utafiti Naliendele kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanya utafiti wa awali na kubaini kuwa ugonjwa huo wa MNYAUKO FUSARI unasababishwa na vimelea aina ya ukungu (fungus) viitwavyo ***Fusarium oxysporum*** ambavyo husababisha mti wa mkorosho kukauka. Aidha, ugonjwa huo husambaa kwenye udongo (soil born disease) na pia unaweza kusambazwa kwa njia ya vitendea kazi, vipando vya mikorosho vilivyoathirika na kuni za mikorosho iliyoambukizwa.

**Dalili za ugonjwa huo ni:**

- Majani kuwa rangi ya njano na hatimaye kahawia;
- Uozo wa kikahawia kwenye kiini cha mti hatimaye mti kukauka kabisa.

**Athari za ugonjwa:**

- Kupungua kwa idadi ya mikorosho na hatimaye uzalishahaji kupungua;
- Mikorosho kufa
- Kupungua kwa pato la mkulima na Taifa kwa ujumla.

**Maeneo yaliyoathirika na ugonjwa:**

Baadhi ya maeneo ambayo ugonjwa umeonekana ni pamoja na Magawa (Mkuranga), Nanganga (Masasi), Nakayaka na Mweru

(Tandahimba), Mtawanya (Mtwara) na Legezamwendo (Liwale) kama ilivyooneshwa kwenye jedwali.

**Maeneo yaliyoonekana kuwa na ugonjwa huo hadi Februari, 2018**

| Mkoa | Wilaya | Kata | Kijiji | Mwaka | Miti iliyoathirika |
|---|---|---|---|---|---|
| Pwani | Mkuranga | Magawa | Magawa | 2012 | 523 |
| | | | Makumbea | 2017 | 6 |
| Mtwara | Masasi | Nangoo | Nangoo | 2014 | 73 |
| | | Nanganga | Nanganga | 2014 | 76 |
| | | Mpindimbi | Kachepa | 2015 | 6 |
| | | Dinduna | Tandika | 2015 | 30 |
| | | Mdumbwe | Nambamba | 2016 | 3 |
| | Tandahimba | Chikongola | Nakayaka | 2017 | 10 |
| | | Chaume | Mweru sokoni | 2017 | 6 |
| | Mtwara vijijini | Mnongodi | Kiwengulo | 2015 | 40 |
| | | Nanyamba | Nanyamba | 2016 | 6 |
| | Mtwara mjini | Mangamba | Mangamba | 2017 | 7 |
| Lindi | Liwale | Liwale B | Legezamwendo | 2018 | 130 |
| **3** | **6** | **12** | **13** | | **916** |

## HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA WIZARA

Taasisi ya Utafiti Naliendele kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar esa Salaam, imeshaanza kufanya utafiti. Utafiti huo unalenga kubaini viuatilifu, mbegu zenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huo. Tafiti zimeanzishwa katika baadhi ya maeneo ambayo ugonjwa umeonekana ambayo ni pamoja na Magawa (Mkuranga),

Nanganga (Masasi), Nakayaka na Mweru (Tandahimba), Mtawanya (Mtwara) na Legezamwendo (Liwale).
Kutoa taarifa kwa wadau kuhusu uwepo wa ugonjwa katika Wilaya za Mikoa ya Pwani, Mtawara na Lindi.

**HATUA ZINAZOTARAJIWA KUCHUKULIWA NA WIZARA**

- Kuendelea na utafiti ili kubaini viuatilifu
- Kufanya tafiti za kiikolojia
- Kufanya tafiti za kibaiyolojia
- Kuendelea na utafiti wa kupata mbegu zenye ukinzani
- Kuendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu utafiti wa namna ya kudhibiti ugonjwa huo
- Kuzishirikisha Taasisi au Maabara za Kimataifa (CAB International, NRI)
- Kuendelea kutoa elimu kwa wadau jinsi ya kudhibiti ugonjwa huo
- Kuendelea kutafuta taarifa za kuwepo kwa ugonjwa huo katika maeneo mapya

**MAMBO YA KUZINGATIWA NA WAKULIMA ILI UGONJWA USIENEE**

Baada ya kuona dalili kama nilivyoeleza hapo juu, wakulima wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Kukata miti iliyoathirika kwa ugonjwa huo na kuichoma moto;
- Kabla hawajakata au kupogolea matawi ya mikorosho isiyoathirika na ugonjwa huo wahakikishe vitendea kazi walivyotumia katika mikorosho iliyoathirika vimebabuliwa na moto.
- Mabaki ya mikorosho iliyoathirika isitumike kama kuni;

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo napenda kusema kuwa, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kuwa uzalishaji na tija ya zao la korosho unaimarishwa ikiwa ni pamoja na mazao mengine ya kimkakati. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki za kuimarisha usimamizi wa uzalishaji wa mazao hayo ili yaweze kutoa mchango mkubwa katika kulipatia Taifa pato la kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara inapenda kusisitiza kuwa wakulima wachukue tahadhari kuhusu ugonjwa huo kwa kuhakikisha kuwa wanazingatia ushauri wa wataalam wa namna ya kudhibiti ugonjwa huo. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utafiti unaondelea ili kupata ufumbuzi wa ugonjwa huu.

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**Wizara ya Kilimo** **Dodoma, Aprili 2018**